

ABDULRAHMAN AL-SUMAIT UNIVERSITY (SUMAIT),



TANGAZO LA ZABUNI YA HUDUMA ZA USAFI NA BUSTANI

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait (**SUMAIT**) kilichopo katika maeneo ya Chukwani, Mkoa wa Mjini Magharibi - Wilaya ya Magharibi 'B' ya Unguja unakaribisha maombi ya huduma za usafi na bustani kutoka kwenye Taasisi /Mashirika/Makampuni na watu binafsi wenye uwezo, leseni, uzoefu na sifa za kutoa huduma ya Usafi na Bustani kwenye Kampasi za Chuo Kikuu cha SUMAIT na Dahalia za wanafunzi pamoja na makaazi ya wafanyakazi wake kwa kipindi cha kuanzia June 01, 2023 hadi May 31, 2024. Huduma hizi zinahitajika zitolewe kwa weledi wa hali ya juu pamoja na kutunza na kuimarisha bustani za chuo hichi.

2. MAENEO YANOYOHITAJI HUDUMA ZA USAFI NA BUSTANI

Maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya kupatiwa huduma za usafi na bustani ni:

1. Huduma za usafi na kuimarisha bustani zinahitajika katika maeneo yote yanayo zunguka Chuo Kikuu cha SUMAIT, Maeneo ya Ndani na nje ya majengo yote yanayozunguka Chuo Kikuu.
2. Eneo la Msikiti wa Chuo Kikuu pamoja bustani zake zote.
3. Eneo la ndani na nje ya Kituo cha Afya (Al-Hijri Dispensary) Pamoja na mazingira ya skuli ya Chekechea iliyomo ndani ya Chuo.

4. Madarasa yote yakusomea wanafunzi wa Chuo, Madarasa makubwa ya kufundishia, Vyoo vyote vilivyomo chuoni pamoja Maktaba za Chuo, Laboratories na Ofisi zote zilizomo ndani ya chuo cha SUMAIT.
5. Dahalia zote za wanafunzi wa kike na kiume pamoja na makaazi ya wafanyakazi wa chuo cha SUMAIT.

4. KANUNI ZA MAOMBI KWA HUDUMA ZA USAFI NA BUSTANI

Waombaji wote wa huduma za usafi na bustani waliotimiza masharti na kuwa na sifa za kutoa huduma hizi wanatakiwa kukamilisha mambo yafuatayo katika maombi yao.

Maombi yatakwawasilishwa yawe pia na taarifa muhimu za mwombaji zifuatazo: -

- Anuani, Mahali Ofisi ilipo, Namba ya simu na E-mail,
- Vifaa vya usafi alivyo navyo kwa kazi aliyoomba pamoja na vya bustani,
- Wafanyakazi na Wataalamu alionao (Elimu na ujuzi wao),
- Uwezo wa kifedha utakaohitishwa na benki
- Uzoefu alionao katika utoaji wa huduma za usafishaji na bustani.
- Malipo ya mshahara ya kila mwezi kwa wafanyakazi wake.

Vile vile Mwombaji wa kazi hii atatakiwa kuambatanisha katika maombi yake nakala za vielelezo vifuatavyo; -

- Taarifa za muongozo wa Taasisi/ Kampuni ya usafi na Bustani (Company Profile).
- **Kibali cha biashara au Taasisi (Business License)**
- Cheti cha usajili wa TIN (TIN certificate)
- Cheti cha usajili wa Mlipa Kodi (VAT registration certificate)
- Kibali cha Usajili wa Taasisi/Kampuni (Company registration Certificate)
- Kibali cha usajili wa Taasisi/Kampuni (Certificate of Incorporation)

5. UWASILISHAJI WA ZABUNI

Maombi yote huduma za bustani na usafi yanaweza kutumwa kwa njia ya kuwasilisha ofisini au kwa email ya chuo cha SUMAIT na yatumwe kwenye bahasha iliyoandikwa; - Habari “**MAOMBI YA HUDUMA ZA USAFI NA BUSTANI KATIKA CHUO KIKUU CHA ABDULRAHMAN AL-SUMAIT (SUMAIT) CHUKWANI – ZANZIBAR**”.

Mwombaji atume maombi yake kwa kuambatanisha na vitu vifuatanavyo:-

- a. Barua ya maombi iliyosainiwa.

- b. Akiambatanisha na maelezo binasfi ya muombaji akionesha mawasiliano na wapi anapatikana.
- c. Akionesha uongozi wa Taasisi au Kampuni yake.
- d. Barua za wadhamini wa muombaji

2. Kwa wale watakaotuma kwa njia ya kieletroniki watume katika katika barua pepe ya Chuo Kikuu cha Sumait. Yenye kichwa cha Habari **“MAOMBI YA HUDUMA ZA USAFI NA BUSTANI KATIKA CHUO KIKUU CHA SUMAIT CHUKWANI – ZANZIBAR”**.

3. Maombi yote yawasilishwe katika Anuwani ya chuo cha SUMAIT na barua pepe iliyopo hapa chini si zaidi ya tarehe **25.05.2023**, au unaweza kutuma maombi yako katika barua pepe hii hapa: recruitment@sumait.ac.tz

Makamo Mkuu wa Chuo Kikuu
Abdulrahman Al-Sumait University (SUMAIT)
S.L.P 1933
Chukwani
Zanzibar

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **25.05.2023**